# KAULI YA DR. SALIM AHMED SALIM DHIDI YA KASHFA NA SHUTUMA DHIDI YAKE COURTYARD HOTEL SAA 4.00 ASUBUHI TAREHE 23/4/2005

Hivi karibuni zimejitokeza juhudi za makusudi za kunikashifu na kujaribu kunichafulia jina langu. Juhudi hizi zinaonekana kuhusishwa na uamuzi wangu wa kuomba kuteuliwa kama mgombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi.

Uchafuzi huu wa makusudi umekuwa ukifanywa kupitia baadhi ya vyombo vya habari, na kwa kasi ya aina pekee kupitia vikundi vya watu waliopita na wanaoendelea kupita mikoani na wilayani wakitupa shutuma za kashfa nzito dhidi yangu familia yangu, uzalendo wangu na hata uhuru wangu.

Nilitafakari kwa muda mrefu kama kuna haja ya kusema lolote hasa kwa vile ni imani yangu kwamba Watanzania wenzangu wanayaelewa fika mema yangu na mapungufu yangu; na kwamba kwa mantiki hiyo hawatakubali kudanganywa au kuyumbishwa kwa uzushi na fitna. Lakini hapo hapo naelewa funzo la kihistoria kwamba uongo ukirudiwarudiwa mara kwa mara unaweza kuanza kutia wasi wasi na kubabaisha. Kwa hiyo hata kama ingekuwa hakuna zoezi hili la uchaguzi ningepeswa kufafanua kuhusu shutuma kama hizo.

Pamoja na kwamba zipo shutuma kadhaa, sikusudii kuzigusia zote.
Hapa nitataja tu shutuma zile ambazo hurejewa mara kwa mara. Shutumai nzito kuliko zote ni zile zinazodiriki kunihusisha kwa namna moja au nyingine na mauaji ya Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume mwaka 1972. Wanaotoa shutuma na uzushi huo wanajua fika kwamba mimi kamwe sikuhusika wala nisingehusika na uhalifu huo. Wanaotoa uzushi huo bila ya shaka wanafanya hivyo kwa lengo la kunichafulia jina langu. Ni jambo la kushangaza na kuhuzunisha sana kuona kuwa licha ya misingi madhubuti tunayojivunia katika Taifa letu, bado shutuma nzito kama hizi zinaweza zikatolewa kiholela na hata kuchapishwa katika magazeti.

Mimi niliteuliwa kuwa Balozi kwenye Umoja wa Mataifa mwaka 1970 na nilikuwa huko hadi 1980. Mzee Karume aliuawa tarehe 7 April 1972. Siku hiyo mimi nilikuwa niko Conakry, Guinea nikiongoza mkutano wa Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Mataifa ambayo mimi nilikuwa mwenyekiti wake. Kifo hicho kilitushtusha, kilitusikitisha na kutuhuzunisha sote tuliokuwepo huko Conakry kama kilivyowashtusha, kuwasikitisha na kuwahuzunisha

mamilioni ya Watanzania wenzangu. Kwa vile nilikuwa naongoza Kamati ambayo ilikuwa inatembelea nchi kadha za Afrika, kutoka Conakry, tulikwenda Lusaka na baadae kupitia Dar es Salaam.

Baada ya ziara hiyo, nimekuwa nikirudi mara kwa mara Tanzania – Bara na Zanzibar kwa kipindi chote cha miaka ya Sabini na wakati wote huo sijashutumiwa wala kuhojiwa.

Mwezi Novemba, 1980 Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje. Kama kweli kulikuwa na shutuma za namna hiyo ingeingiaje akilini mwa Marehemu Mwalimu Nyerere kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa miaka mine na Viongozi wa Zanzibar nao wakae kimya?. Si hivyo tu, baadaye Mwalimu aliniteua kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania. Sasa suala la kujiuliza ni: Kama mimi ningehusika kwa namna yeyote ile na uhalifu huo, Je! Baba wa Taifa ambaye lazima alikuwa na taarifa zote juu ya mauaji hayo angeniteua kuwa Waziri Mkuu wake na kabla ya hapo kunipigia debe nilipowania Ukatibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa? Inaingiaje akilini kwamba Mwalimu Nyerere amteue mtu mwenye tuhuma nzito kama hizo kuwa Waziri wake Mkuu. Hivyo ndivyo tunavyomuenzi Baba wa Taifa letu? Ingeyumkinikaje kwa Rais wa Awamu ya Pili, Mzee wetu, Al Haj Ali Hassan Mwinyi anayetoka Zanzibar, naye kuniteua mimi kushika Wizara nyeti kama ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na baadaye yeye na Viongozi wengine wa Taifa letu kufanya kila jitihada ili nichaguliwe kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa nchi Huru za Afrika? Kama ningekuwa na tuhuma hizo, ingeingia akilini mwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Rais Benjamin Mkapa kuniteua kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa mara tu baada ya kurejea nyumbani, baada ya kumaliza muda wangu kama Katibu Mkuu wa OAU?

Ningependa kukumbusha pia kwamba kabla sijaenda Addis Ababa kwa muda wa miaka tisa nilikuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Katika kipindi hicho nilikuwa Mkuu wa Idara ya Mambo ya Nje ya Chama na kwa miaka mitatu nilikuwa pia Katibu wa Tume ya Ulinzi na Usalama.

Ni jambo lililo dhahiri kwamba tuhuma hizo zinazoendelezwa kisirisiri na bayana ndani ya baadhi ya vyombo vya habari ni uzushi na uongo mtupu na wenye lengo moja tu la kunichafulia jina langu wakati huu wa zoezi la kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya CCM. Tujiulize: kutoa shutuma nzito kama hizo ambazo zinahusu hata usalama wa Taifa letu kwa madhumuni tu ya kumpaka mtu matope una faida gani kwa nchi

na jamii yetu? Nini thamani ya Urais utakaopatikana kwa kuwashambulia, kuwazulia na kuwashutumu wasio na hatia yeyote?

Jambo jingine linalosemwa ni lile la rangi yangu na "Uarabu" wangu. Inashangaza kwamba katika karne hii ya 21 na tukizingatia misingi ya Chama chetu cha Mapinduzi bado wapo watu ambao wangetaka kutumia rangi na ukabila kuwa ndio vigezo vya kupata uongozi. Hapa ningependa tujikumbushe mambo mawili ya msingi: Kwanza, Chama chetu (CCM) daima kimesimamia haki na kupinga ubaguzi wa aina yeyote ndani na nje ya nchi. Pili, Tanzania ni Taifa ambalo limejivunia rekodi yake ya kuwa mstari wa mbele kupinga ubaguzi wa rangi, ukabila, udini na uonevu wa aina yeyote ndani ya bara letu na duniani kwa jumla.

Mimi mwenyewe katika nyadhifa mbalimbali ambazo nimewahi kushika ndani na nje ya nchi nimekuwa muaminifu na muadilifu katika kutekeleza sera ya Taifa letu katika jambo hilo. Hivi sasa mimi nawakilisha Bara la Afrika katika Kikundi Andamizi cha watu watano mashuhuri duniani ambao wameteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kusimamia utekelezaji wa Maamuzi ya Mkutano wa Viongozi wa Dunia uliofanyika Durban miaka mine iliyopita, ili kupambana na ubaguzi wa rangi na aina zote za ubaguzi.

Na huu "Uarabu" wangu unaonekana leo? Nimelitumikia Taifa langu kwa miaka 41 katika nyadhifa mbali kwa uadilifu na uaminifu. Nimefanya hivyo kama Mtanzania na kama Mwafrika. Wakati wote huo hakuna aliyeutilia mashaka Uzalendo wangu wala Uafrika wangu! Viongozi Wakuu wa Umoja wa Afrika kwa kutambua mchango wangu nilioutoa katika Bara letu walinitunukia medali ya dhahabu kule Durban mwezi wa Julai, mwaka 2002. Viongozi hao walinipa tuzo kwa utumishi uliotukuka, kwa niaba ya Waafrika wa Bara letu Watanzania wakiwemo. Rais Thabo Mbeki kwa upande wake, na kwa niaba ya wananchi na Serikali ya Afrika ya Kusini, mwaka jana alinitunukia Nishani ya dhahabu kama rafiki mkuu wa Marehemu Oliver Tambo kwa uongozi niliouonyesha na mchango nilioutoa katika harakati za kukomesha ukoloni katika Bara la Afrika. Ilikuwa ni heshima ya pekee kwangu kuwa Mtanzania wa pili baada ya Marehemu Mwalimu Julius Nyerere kutunukiwa nishani hiyo. Lakini leo licha ya yote hayo, kwa sababu naomba nafasi ya uongozi wa Taifa ghafla kuna wachache kwa sababu zao wenyewe wanaotaka kutuyumbisha.

Kuhusu suala hili la ukabila ningependa kuongeza jambo moja tu. Mimi ni kweli mchanganyiko wa damu ya Kiarabu, Kinyamwezi na Kimanyema. Mimi ni Mzanzibari na ni Mtanzania na kuna wengi miongoni mwa Wazanzibari wakiwemo viongozi wenye hali kama hiyo.

Lakini tokea lini kigezo cha Chama chetu au Taifa letu kikawa katika misingi hiyo. Tunakwenda wapi?

Tangu tupate Uhuru Watanzania tumeonyesha kwa vitendo kwamba ubaguzi hauna nafasi nchini kwetu. Wananchi wa Kinondoni na Watanzania kwa ujumla wanakumbuka utumishi na uongozi bora wa marehemu Derek Bryceson. Vivyo hivyo wananchi wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla wanakumbuka utumishi uliotukuka wa marehemu Amir Jamal. Wote wawili walichaguliwa na kuchaguliwa tena bila kujali rangi yao. Tunakumbuka pia utumishi wa kutukuka uliotolewa na marehemu Leader Stirling na Mzee Al Noor Kassum na wengineo.

Hata sasa tuna viongozi wengi wa rangi na kabila mbali mbali katika serikali zetu mbili, ndani ya Bunge na ndani ya Baraza la Wawakilishi. Tukianza ubaguzi kwenye kugombea urais, dhambi hiyo, kama alivyosema Mwalimu Nyerere, haitaishia hapo. Itaendelea kwenye uchaguzi wa wabunge, wawakilishi na madiwani. Tutabaguana kwenye siasa na ndani ya jamii. Tutabaguana siyo kwa rangi bali pia kwa ukabila na dini. Tutakuwa tumevunja msingi mkubwa wa umoja wa taifa letu, msingi ambao umejenga amani, utulivu na mshikamano wa Watanzania.

Shutuma nyingine inayosambazwa ni kuwa ndugu zangu wote wako huko katika Ghuba na hasa Oman. Huo ni uzushi, na wanaozua wanajua fika kwamba huo ni uongo mtupu. Mwenyezi Mungu alitubariki kuwa na familia kubwa. Baadhi ya wadogo zangu wamefariki. Waliohai, Watano wako hapa Tanzania, Wawili wako Denmark, mmoja yuko Kenya (Mombasa), mwingine yupo Canada, mmoja yupo Botswana na wanne wako huko Ghuba. Lipi la ajabu? Tokea lini jambo kama hili likawa kigezo cha Chama chetu au Taifa letu? Kiongozi kuwa na ndugu nje ya nchi ni dhambi? Je hakuna Mtanzania aliye na ndugu nje? Na akiwa nao utanzania wake unapungua? Tunakwenda wapi?

Shutuma nyingine inayosambazwa ni kwamba nilipokuwa OAU sikuwasaidia Watanzania! Hapa napenda nikumbushe yale niliyoyasema pale Mgulani kabla sijaenda Addis Ababa kuchukua nafasi hiyo ya Ukatibu Mkuu katika karamu ya kuniaga iliyoandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Nilisema nakwenda Addis Ababa kutumikia bara lote la Afrika. Ukiwa Katibu Mkuu, maana yake ni kuwa mtumishi wa nchi zote za Bara la Afrika; na si Katibu Mkuu wa Tanzania. Kwa miaka kumi na miwili na kwa vipindi vitatu mfululizo, nilijitahidi kwa uwezo wangu wote kulitumikia bara letu bila ya

upendeleo. Na ndio maana viongozi wakuu wa Afrika waliniamini na kuendelea kunipa heshima hiyo. Sisemi kwamba kila nililolifanya lilikuwa sahihi. Lakini najivunia kwamba wakati wote niliposhika nafasi hiyo nilijitahidi kwa kikomo cha uwezo wangu wote kutekeleza majukumu yangu.

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kutumikia Taifa langu katika nafasi mbalimbali. Nimepata faraja kubwa sana kwa heshima niliyopewa na Chama changu na Taifa langu katika miaka yote hii. Marehemu Mzee Karume aliniteua kuwa Balozi wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar huko Cairo, Misri nikiwa kijana wa miaka 22. Alifanya hivyo si kwa kubahatisha au kwa upendeleo maalum. Mzee Karume alitambua mchango wangu katika vugu vugu la kupigania Uhuru wa Zanzibar. Nilifanya kazi naye kwa karibu wakati yeye akiwa Mwenyekiti na mimi nikiwa Katibu Mtendaji wa Umoja wa Vyama vya Upinzani (UNITED FRONT OF OPPOSITION PARTIES) ambao ulishirikisha Afro-Shirazi Party, Afro-Shirazi Youth League, Umma Party, Umma Youth, Zanzibar and Pemba Federation of Labour, Federation of Progressive Trade Unions, All Zanzibar Journalists Organization na All Zanzibar Students Union. Wakati huo mimi pia nilikuwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la Vyama hivyo vya Upinzani.

Ni muhimu kuwa wakweli wa historia. Kwani tukibadilisha au kupinda pinda historia kwa utashi wa mtu au kundi la watu binafsi kuna hatari kwamba kila kizazi kitajiandikia historia yake kwa maslahi yake, na hiyo haitakuwa historia tena!

Mwisho ningependa kusisitiza kuwa katika kugombea nafasi hii kuna kushinda au kutoshinda. Mimi nimejitayarisha kwa yote mawili. Lakini kwa vyovyote vile ni imani yangu kwamba wana CCM watakaokutana huko Dodoma tarehe 2, 3 na 4 mwezi Mei, 2005, watanihukumu kwa kuzingatia utumishi wangu kwa Taifa letu, kwa uadilifu wangu, uaminifu wangu na uwezo wangu na sio kwa tuhuma na shutuma za kupachikwa na wale wasionitakia mema. Yeyote atakayechaguliwa miongoni mwetu atahitaji msaada na ushirikiano wa wenzake wote. Nawaomba Watanzania tuwe makini. Tusiyumbishwe wala kupotoshwa.

Asanteni kwa kunisikiliza
**23/4/2005**
**Dar es Salaam**